



## Njia ya Sindano

Sindano ni njia ya uzazi wa mpango inayotolewa kila baada ya miezi mitatu. Sindano hii ina kichocheo cha projestin, ambacho kinafanana na kichocheo cha asili alichonacho mwanamke ambacho hutoka kidogo kidogo mwilini.

- Ni salama na ina ufanisi mkubwa
- Haina madhara kwka unyonyeshaji. Inaweza kutumika mara baada ya kujifungua
- Inasaidia kujikinga na saratani ya kizazi na uvimbe
- Mabadiliko ya mpangilio wa hedhi yanaweza kutokea kwa baadhi ya watumiaji nayo ni;
  - o Kuvurugika au hedhi za muda mrefu kwa miezi mitatu ya mwanzo
  - o Kukosa kabisa hedhi, kupata hedhi bila mpangilio wa mara kwa mara
- Mwanamke mwenye VVU, UKIMWI au anayetumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI anaweza kutuumia njia hii ya sindano
- Mwanamke mwenye VVU anatakiwa kutumia kondomu ili kuzuia maambukizi mapya ya VVU au magonjwa ya ngono
- Matumizi ya sindano YANAWEZA kuongeza uwezekano wa kupata maambukizi ya VVU. Wanawake wanaotaka kutumia sindano wanaweza kupunguza uwezekano huo kwa kutumia kondom kwa usahihi kila wakati